JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS

TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

HOTUBA YA MHE. STEPHEN N. KAGAIGAI,

MKUU WA MKOA WA KILIMANJARO WAKATI WA KUWAAPISHA WAKUU WA WILAYA WATEULE

TAREHE 22 JUNI, 2021

Imetayarishwa na:
Ofisi ya Mkuu wa Mkoa,
Kilimanjaro,
S.L.P. 3070,
MOSHI.

Simu: +255 027 2758248/027 2751381
Barua Pepe: *ras@kilimanjaro.go.tz*
rc@kilimanjaro.go.tz

JUNI, 2021

HOTUBA YA MHE. STEPHEN N. KAGAIGAI, MKUU WA MKOA WA KILIMANJARO WAKATI WA KUWAAPISHA WAKUU WA WILAYA WATEULE

TAREHE 22/06/2021

ITIFAKI:

- Mheshimiwa Mwenyekiti wa CCM Mkoa;
- Ndugu, Katibu Tawala wa Mkoa;
- Waheshimiwa Wakuu wa Wilaya;
- Wajumbe wa Kamati ya Usalama ya Mkoa;
- Mheshimiwa Mstahiki Meya wa Manispaa ya Moshi;
- Waheshimiwa Wenyeviti wa Halmashauri;
- Ndugu Makatibu Tawala wa Wilaya;
- Ndugu Wakurugenzi wa Halmashauri;
- Waheshimiwa Viongozi wa Dini
- Ndugu Wataalamu wa Sekretarieti ya Mkoa;
- Waandishi wa Habari;
- Mabibi na Mabwana.

Nawasalimia kwa Jina la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

SALAMU ZA PONGEZI:

Waheshimiwa Wakuu wa Wilaya,

- Nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa wema wake kwa nchi yetu

- Mwenyezi Mungu pia amewezesha kuwepo kwa utaratibu mzuri na endelevu wa kubadilisha na kurithishana madaraka kwa amani na utulivu kama ambavyo sheria, kanuni na taratibu zinavyotutaka.

- Aidha, nachukua fursa hii kuwapongeza kwa kukubali uteuzi huuna hatimae kushiriki katika tukio hili la kiapobaada ya kuteuliwa na Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kushika wadhifa huu Mkuu katika Wilaya zetu za Mkoa wa Kilimanjaro.**Hongereni sana.**

Binafsi nampongeza Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuwateua kuwa Wakuu wa Wilaya. Hii imedhihirisha Imani kubwa aliyo nayo kwenu. Hivyo nawasihi, kwa pamoja tushirikiane kumsaidia kusimamia amani, utulivu na shughuli za Maendeleo ya wananchi ambazo ndio kazi zetu za msingi.

KUSIMAMIA UTAWALA BORA

Waheshimiwa Wakuu wa Wilaya;

- Hivi punde mmekula kiapo kinachoambatana na kazi zenu za Ukuu wa Wilaya.

- Nitumiefursa hii kusisitizakuzingatia mambo yafuatayo ili kulinda Kiapo chenu: -
  1. Kasimamieni misingi ya haki, utawala wa sheria na maadili katika kutekeleza majukumu yenu.

  2. Kasimamieni amani na Usalama wa wananchi na mali zao. Mtambue kwamba nyie ndio Wenyeviti wa kamati za Usalama katika ngazi za wilaya mkisaidiwa na vyombo vya Usalama.
     - Nendeni mkashirikiane navyombo vya Usalama, kupitia kamati ya usalama katika kufanya maamuzi makubwa ya Wilaya. Aidha, sambamba na kamati ya Usalama, ni vizuri kushirikiana pia na Viongozi wa Kisiasa, Dini, wananchi na wadau wengine katika kudumisha amani.

  Nendeni mkawe viungo katika Wilaya zenu kwani Uongozi ni kuwa kiungo/Daraja muhimu katika jamii.

UTATUZI WA KERO ZA WANANCHI

Waheshimiwa Wakuu wa Wilaya,

- Kama viongozi mnayo kazi ya kusikiliza na kutatua kero mbalimbali za wananchi katika maeneo yenu ya Kiutawala.

- Ni vema tuhakikishe tunazielewa kero za wananchi na kuzitatua kwa weledi, uadilifu na bila ubaguzi wala upendeleo wowote.

  Nitoe rai kwenu kwenda kujipanga vizuri kwa kushirikiana naMakatibu Tawala wa Wilaya, Wakurugenzi wa Halmashauri na Wakuu wa Taasisi zilizo katika Wilaya zenu kuhakikisha kwamba madawati ya kusikiliza kero za wananchi yanakuwepo na yanafanya kazi.

KUSIMAMIA SHUGHULI ZA MAENDELEO

Waheshimiwa Wakuu wa Wilaya;

- Tambueni kwamba mnalo jukumu kubwa la kuzisimamia Halmashauri ili kuhakikisha kwamba zinatekeleza majukumu yake kwa kuzingatia Sheria na miongozo ya Serikali.

- Kasimamieni pia, suala zima la Ukusanyaji wa mapato ya Halmashauri naKuhakikisha mapato haya yanatumika kwa ajili ya shughuli za maendeleo ya wananchi

- Aidha, simamieni pia udhibiti wa matumizi ya fedha za Serikalina kuzuia ubadhilifu, ikiwa ni pamoja na kuwachukulia hatua wale wote waliokiuka taratibu. Hili lifanyike kwa kuzingatia sheria na miongozo iliyopo pamoja na Kanuni.

- Hakikisheni sehemu ya mapato ya Halmashauri yanaelekezwa kwenye miradi ya maendeleo kwa kadri ya bajeti za Halmashauri na miongozo.
- Fuatilieni kwenye Halmashauri kuhakikisha asilimia ya bajeti inatolewa kwa makundi maalum yakiwemo ya wanawake, vijana na wenye ulemavu.

KASIMAMIENI SUALA ZIMA LA UWEKEZAJI

NA KUKUZA FURSA ZA AJIRA

Waheshimiwa Wakuu wa Wilaya,

- Nendeni mkafanye kazi ya Katafuta wawekezaji. Kwa kufanya hivi mtakuwa mmepata muarobaini wa upatikanaji wa Ajira hususan kwa Vijana wetu.

- Aidha, naomba niwakumbushe pia kwamba, kwa sasa taifa limejikita katika kuimarisha njia kuu zauchumi, kilimo, viwanda, usafirishaji na mawasiliano. Mambo haya yapo katika ngazi zote za uongozi. Ninategemea kuona ubunifu wenu wa hali ya juu katika kuimarisha sekta hizi pamoja na sekta za huduma kama: elimu, afya, maji, biashara, n.k.

- Fanyeni ubunifu wa kuwahamasisha vijana kupenda na kufanya kazi tofauti na ilivyo sasa ambapo vijana wengi wamejikita kwenye masuala yasiyo na tija kwa maisha yao.

SHUKRANI NA HITIMISHO

Ndugu Viongozi na Wataalam;

- Napenda kuhitimisha hotuba yangu kwa kuwaomba kila mmoja kwenda kusimamia suala nzima la kiafya hususan tahadhari ya ugonjwa wa Corona kwa kuzingatia miongozo na tahadhari zote zinazotolewa na Wizara ya Afya.

- Twendeni tukasimamie misingi ya Afya ili sisi na watu wote tuwe salama na wimbi hili lituache salama.

- Nawashukuru viongozi wa dini kwa kuwa nasi bega kwa bega mara zote pale tunapowahitaji, lakini pia kuliombea Taifa letu kwa nyakati mbalimbali, nawaomba tuendelee kufanya hivyo kwa vile Taifa letu linawategemea sana.

- Napenda pia kuwashukuru Viongozi wa Kisiasa na hasa wale wa Chama Tawala cha CCM kwa ushirikiano wenu.

- Mwisho, nawashukuru sana kwa kunisikiliza na ninawatakia waheshimiwa Wakuu wa Wilaya kila la kheri katika kutekeleza majukumu yao.

Asanteni sana kwa kunisikiliza!